JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

TAARIFA KWA UMMA

UFAFANUZI KUHUSU ADHABU YA MGOMBEA WA KITI CHA RAIS KWA TIKETI YA CHADEMA

Dar es Salaam, 03 Oktoba, 2020

Kumekuwa na tafsiri isiyokuwa sahihi kuhusu adhabu iliyotolewa na Kamati ya Maadili ya Kitaifa jana tarehe 2 Oktoba, 2020 dhidi ya mgombea wa kiti cha Rais kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Bw. Tundu Antiphas Lissu kwa baadhi ya watu kutaka kuaminisha umma wa watanzania kwamba mgombea huyo ameadhibiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Ukweli ni kwamba, Bw. Lissu ameadhibiwa na Kamati ambayo inajumuisha wawakilishi wa vyama vyote vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi wa kiti cha Rais. Hivyo basi, wajumbe 15 kutoka vyama vya ADA-TADEA, CUF, SAU, UPDP, CHADEMA, CHAUMMA, CCM, NCCR-Mageuzi, DP, UMD, ACT-Wazalendo, NRA, Demokrasia Makini, ADC na AAFP ndio waliotoa adhabu kwa Bw. Lissu. Aidha, Kamati pia ina mjumbe mmoja kutoka Serikalini na Mjumbe wa Tume ambaye kwa muundo wa Kamati yeye ndio alikuwa mwenyekiti. Ifahamike kwamba katika kikao hicho kulikuwa na mawakili wawili kutoka CHADEMA waliosimama kutetea hoja ya Bw. Lissu mbele ya Kamati.

Kwa kuzingatia adhabu zilizoanishwa katika kanuni ya 5.11 ya Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2020, mgombea huyo amepewa adhabu ya

kutofanya kampeni kwa siku 7 kuanzia tarehe 3 Oktoba hadi tarehe 9 Oktoba 2020. Hii ina maana kuwa haruhusiwi kufanya kampeni yake au kwa ajili ya mgombea mwingine.

Endapo mgombea huyo atadharau uamuzi wa Kamati na kufanya kampeni atambue kuwa, Kamati imepewa mamlaka ya kuelekeza makosa mengine kwenye vyombo vingine kadri itakavyoona inafaa kama ilivyoinishwa kwenye kanuni ya 5.7 (l) ya Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2020. Ikumbukwe kuwa, kipindi cha uchaguzi sheria nyingine za nchi hazijaacha kufanya kazi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kushauriana na vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu pamoja na Serikali wanatakiwa kuandaa Maadili ya Uchaguzi pamoja na kuweka utaratibu wa kutekeleza Maadili hayo. Kwa mara ya kwanza Maadili yenye nguvu ya kisheria yalitungwa na kuanza kutumika mwaka 2010. Maadili hayo yaliandaliwa tena mwaka 2015 na mwaka huu 2020 vyama vyote 19 vilishiriki kuyaandaa na baadaye kusaini Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2020 mnamo tarehe 27 Mei 2020.

Sehemu ya Tano ya Maadili ya Uchaguzi inatoa mamlaka ya kuunda kamati za maadili kuanzia ngazi ya kata hadi rufaa. Wajumbe wa kamati hizo hupendekezwa na vyama vya siasa, Serikali na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Kama ilivyoelezwa jana katika taarifa ya Kamati, malalamiko dhidi ya mgombea yalipokelewa, na Katibu Mkuu wa CHADEMA alipewa taarifa kwa maandishi kwa kuzingatia utaratibu ambao vyama vya siasa na Tume walikubaliana tangu awali. Inashangaza kusikia Bw. Lissu akidai apelekewe taarifa yeye mwenyewe kinyume na utaratibu uliowekwa, huku akisahau kwamba tarehe 24 Septemba 2020 alilalamikiwa na Chama cha SAU kuhusu ukiukwaji wa Maadili ambapo barua ilitumwa kwa Katibu Mkuu wa CHADEMA na walijibu kama kawaida.

Kwa kuzingatia taratibu tajwa, Tume hupeleka taarifa kwa Katibu Mkuu wa chama husika kuhusu tarehe ya kuchukuwa fomu za uteuzi na kurejesha, Tume haimpelekei

mgombea mmoja mmoja taarifa, na wagombea kwa kupitia makatibu wakuu wa vyama vyao hupokea taarifa na kujitokeza kuchukuwa fomu na kuteuliwa. Pia, Tume haina na si mtunzaji wa anuani binafsi za wagombea wa nafasi mbalimbali katika uchaguzi. Tume inawasiliana na Katibu Mkuu na si vinginevyo. Hivyo, madai ya Bw. Tundu Lissu kuwa hajapokea taarifa ya malalamiko mpaka leo ni uongo. Chama chake kilipokea taarifa na barua za malalamiko zimentaja kwa jina. Barua ya Katibu wa Kamati ya Maadili ilielekezwa kwa Katibu Mkuu wa CHADEMA kwa kuwa yeye ndiye aliyemdhamini na kumtambulisha Bw. Tundu Lissu kuwa ni mwanachama na mgombea wa kiti cha Rais kupitia CHADEMA kwa mujibu wa matakwa ya ibara ya 39(1)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Ifahamike wazi kuwa Kamati ilifikia uamuzi baada ya majadiliano baina ya walalamikaji na wawakilishi wa CHADEMA, chama ambacho kimemdhamini mlalamikiwa. Hivyo, alipewa taarifa na haki ya kusikilizwa. Adhabu inatakiwa kutekelezwa kwa kuwa imetolewa na chombo chenye mamlaka ya kisheria na kwa kuzingatia taratibu. Mgombea wa kiti cha Rais kupitia CHADEMA anatakiwa kuheshimu na kutekeleza adhabu hiyo kama ilivyotolewa.

Aidha, mgombea amelalamika kuwa malalamiko ya kukiuka Maadili ya Uchaguzi dhidi ya vyama vingine hayatangazwi kama ya kwake. Huu ni upotoshaji wa makusudi, kwani kanuni ya 5.11 (c) ya Maadili ya Uchaguzi, inaainisha kutangaza jina la chama au mgombea aliyekiuka maadili kama sehemu ya adhabu. Suala la Bw. Tundu Lissu limetangazwa kwa sababu ni sehemu ya adhabu aliyopewa na kamati. Kamati si Tume ya Taifa ya Uchaguzi, bali ni chombo kinachoundwa na vyama vyote vyenye wagombea wa kiti cha Rais kikiwemo CHADEMA.

Emmanuel Kawishe

KATIBU
KAMATI YA MAADILI YA KITAIFA